TANGAZO LA SERIKALI NA. 833 la tarehe 2/10/2020

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA

(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Zimetungwa chini ya Kifungu cha 6 (1) na 16 (1)*

SHERIA NDOGO ZA USHURU WA KITUO CHA MAGARI ZA HALMASHAURI YA JIJI LA MBEYA ZA MWAKA, 2020

Jina

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za Ushuru wa Kituo cha Magari za Halmashauri ya Jiji la Mbeya za Mwaka ,2020.

Eneo la kutumika

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Halmashauri ya Jiji la Mbeya.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapoelezwa vinginevyo:-

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote wa Halmashauri aliyeidhinishwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

"chombo cha usafiri" maana yake ni gari la biashara, teksi, bajaji na pikipiki.

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Jiji la Mbeya.

"kituo cha mabasi" maana yake ni eneo lolote lililotengwa na Halmashauri kwa madhumuni ya kupakia na kuteremsha abiria na mizigo.

"mabasi" maana yake ni magari yote yaliyosajiliwa

kufanya biashara ya kusafirisha abiria na mali zao na ambayo yatachukua au kubeba zaidi ya abiria wanne na itajumuisha malori ya aina zote.

“mkurugenzi” maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya pamoja na Afisa yeyote wa Halmashauri atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi.

“maegesho” maana yake ni sehemu maalum iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuegesha magari

“mmiliki” maana yake ni kondakta, dereva au msimamizi wa gari hilo anayelisimamia au kuliendesha likiwa stendi

“teksi” maana yake ni Magari yote yaliyosajiliwa kwa ajili ya kubeba abiria wasiozi sita pamoja na dereva kulingana vna idadi ya viti kama ilivyoainishwa na mamlaka ya leseni katika eneo la Halmashauri.

“ ushuru” maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri na watumiaji wa kituo cha magari.

“wakala:” maana yake ni mtu binafsi, kikundi cha watu,kampuni,au taasisi iliyoteuliwa na Halmashauri kukusanya ushuru kwa niaba yake.

Wajibu wa kuingia stendi

4. (1) Itakuwa ni wajibu wa kila mmiliki wa magari ya abiria na mizigo yatokayo na kwenda nje ya Halmashauri na maeneo yaliyo ndani ya Halmashauri kuhakikisha kuwa magari yao yanaingia katika eneo lililotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kupakia na kushusha abiria na mizigo.

(2) Halmashauri itatoza Ushuru wa stendi kama ilivyoonyeshwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria

Ndogo hizi.

(3) Ushuru wa magari ya abiria na mizigo utalipwa wakati gari linapo kuwa linatoka kituoni kuendelea na safari yake.

Wajibu wa kulipa ushuru

5. (1) Ni wajibu wa kila mmiliki wa gari la abiria au mizigo kulipa ushuru kama inavyoelekezwa katika Jedwali la Sheria Ndogo hizi.

(2) Ushuru unaotozwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi utalipwa kwa Afisa mwidhiniwa au wakala wa Halmashauri ambaye atatoa stakabadhi ya kielektroniki inayolingana na malipo yaliyofanyika.

(3) Kila mtu atakayelipa ushuru chini ya Sheria Ndogo hizi atawajibika kudai na kupewa stakabadhi ya malipo.

Kukusanya ushuru

6. (1) Mmiliki wa gari la abiria au mizigo anaposhindwa au kukataa kulipa ushuru kwa muda unaotakiwa Halmashauri italazimika kukusanya ushuru huo kwa njia ya Mahakama.

(2) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha 6(1) Halmashauri inaweza kukamata gari ambalo mmiliki wake atashindwa kulipa ushuru husika na kulishikilia hadi gari hilo lilipiwe ushuru.

(3) Halmashauri haitawajibika kwa hasara yoyote na kwa namna yoyote itakayotokea ama wakati wa kukusanya ushuru au wa gari lililokamatwa na kushikiliwa, isipokuwa tu kama hasara hiyo itakuwa imesababishwa na uzembe wa watumishi wa Halmashauri.

Marufuku

7. Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote;-

(a)kuosha au kusababisha chombo cha usafiri kuoshwa; au
(b)kutengeneza gari kwenye kituo cha basi

Usajili wa magari

8. (1) Itakuwa ni wajibu wa kila mmiliki wa chombo cha usafiri kwa kuhakikisha kuwa chombo chake anachomiliki kinasajiliwa na Halmashauri.

(2) Kila mmiliki wa chombo cha usafiri atatakiwa kulipa ada ya usajili wa magari kwa mwaka kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hizi.

(3) Maombi kwa ajili ya usajili yatawasilishwa kwa kujaza fomu maalum itakayopatikana kwa Afisa biashara wa Halmashauri.

(4) Itakuwa ni wajibu wa kila mmiliki wa chombo cha usafiri kuhakikisha amebandika stika ya usajili mahali popote ambapo stika hiyo itasoimeka kwa urahisi.

(5) Halmashauri inaweza kufuta usajili wa chombo chochote cha usafiri iwapo mmiliki wake ataenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi.

Rangi ya Teksi

9. Teksi zote zitakuwa na rangi nyeupe, mkanda wa njano katika pande zote mbili pamoja na namba za ubavuni kwa pande zote na alama maalum inayowaka juu ya teksi yenye neno “TAX”.

Makosa

10. Itakuwa ni makosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi iwapo mtu yeyote:-

(a) atakataa au kukwepa kulipa ushuru;

(b) ataosha chombo cha usafiri au kufanya matengenezo makubwa ndani ya kituo cha magari;

(c) atasababisha au kufanya fujo ndani ya eneo la Kituo cha Magari;

(d) atapakia abiria au mizigo katika sehemu isiyo ruhusiwa;

(e) atazuia watumiaji wengine wa stendi kutumia kwa njia yoyote ile;

(f) atamzuia kwa namna yoyote ile Afisa mwidhiniwa kutekeleza majukumu yake;

(g) atashawishi mtu au kundi la watu kukataa kulipa ushuru; au

(h) ataharibu kwa namna yoyote ile vifaa au miundombinu ya Kituo cha Mabasi.

Adhabu

11. Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi laki mbili (200,000/= na isiyozidi shilingi milioni moja (1,000,000/=) au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili (12) na kisichozidi miezi ishirini na nne (24) au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Kufililisha kosa

12. Mkurugenzi anaweza kumtoza mtu yeyote faini isiyopungua shilingi laki mbili (200,000/=) na isiyozidi shilingi laki tano (500,000/=) iwapo mkosaji atakiri kosa kwa hiari yake mwenyewe kwa maandishi na kukubali kutekeleza wajibu wake pamoja na kulipa faini anayodaiwa kama ilivyoelekezwa katika Jedwali la Tatu la Sheria Ndogo hizi.

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetungwa chini ya kifungu cha 4(2))*

**USHURU WA STENDI**

| Na | Aina | Ushuru |
|---|---|---|
| 1. | Basi la abiria zaidi ya 40 | 4000/= kila linapotoka kituoni |
| 2. | Basi la abiria chini ya 40 | 2000/= kila linapotoka kituoni |
| 3. | Basi abiria chini ya 20 | 1500/= kila linapotoka kituoni |
| 4. | Lori la uzito chini ya tani 10 | 2000/= kila linapotoka kituoni |
| 5. | Lori la uzito zaidi ya tani 10 | 4000/= kila linapotoka kituoni |
| 6. | Gari ndogo lisilozidi tani 3 | 1500/= kila linapotoka kituoni |
| 7. | Gari ndogo lisilokuwa la mizigo | 1500/= kila linapotoka kituoni |
| 8. | Pikipiki | 700/= kila inapotoka kituoni |
| 9. | Bajaji | 1500/= kila inapotoka kituoni |
| 10. | Waingia kwa miguu | 200/= kila anapoingia kituoni |
| 11. | Magari mengine yasiyo ya biashara | 1000/= kila inapotoka kituoni |
| | | |

JEDWALI LA PILI

*(Limetungwa chini ya Kifungu cha 8(2)*

ADA YA USAJILI WA MAGARI

| NA. | AINA YA GARI | KIWANGO CHA ADA | MUDA |
|---|---|---|---|
| 1 | BAJAJI | 32,000/= | Mwaka mmoja |
| 2. | PIKIPIKI | 22,000/= | Mwaka mmoja |
| 3. | TEKSI | 50,000/= | Mwaka mmoja |
| 4. | MAGARI YA MIZIGO | 60,000/= | Mwaka mmoja |

JEDWALI LA TATU

*(Limetungwa chini ya Kifungu cha 12)*

HATI YA KUKIRI KOSA

Mimi ………………………………………………… nakiri mbele ya ………………………………… ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya, kwamba, mnamo tarehe ……. ya mwezi ……… mwaka ………… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya Kifungu cha ………… cha Sheria Ndogo za (Ushuru wa Kituo cha Magari) za Halmashauri ya Jiji la Mbeya za mwaka 2020.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya, kwa hiyari yangu niko tayari kulipa Ushuru unaodaiwa pamoja na faini.

Nathibitisha maelezo hapo juu ni ya kweli na nimeyatoa kwa hiari yangu na ufahamu wangu.

Leo tarehe …… ya mwezi …………… mwaka …………
Jina……………………….…………………………
Saini……………

Mbele ya:
Jina……………………………………………….
Cheo ……………………………………………..
Saini ………………

Muhuri wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya Umebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kwa azimio la kikao cha Mkuatano wa baraza la Madiwani uliofanyika tarehe 10/06/2020 na kubandikwa mbele ya;

SAAD A. MTAMBULE
*Kaimu Mkurugenzi*
*Halmashauri ya Jiji la Mbeya*

**LS**

**GIBSON J. MWAKALIBULE**
*Mwenyekiti wa Mkutano*
*Halmashauri ya Jiji la Mbeya*

**NAKUBALI**

DODOMA
05 Agosti, 2020

SELEMANI S. JAFO
*WN OR-TAMISEMI*
DODOMA